**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**

**SHIRIKA LA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA (COASCO)**

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na. CA.61/287/01/24** **15.12.2025**

Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi,
Vyama vya Ushirika,
**TANZANIA BARA**

**YAH: MWALIKO WA MAFUNZO YA SIKU TATU KWA VIONGOZI NA WATENDAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA KUHUSU UHASIBU, UKAGUZI WA NDANI NA MATUMIZI YA 'AI' (21–23 JANUARI 2026).**

Husika na Kichwa cha Habari hapo juu pamoja na barua ya tarehe 24.11.2025 Kumb. Na. CA.61/287/01/3 kuhusu kichwa cha habari hapo juu.

2. Kutokana na sababu ambazo hazikuweza kuzuilika, mafunzo yaliyokuwa yamepangwa kufanyika tarehe 16 hadi 18 Desemba, 2025 yameaihirishwa hadi Januari 2026 kuanzia tarehe 21-23. Aidha, tunaomba radhi kwa usumbusu wote uliotokea kutokana na kuahirishwa kwa mafunzo hayo.

3. Hivyo, programu ya mafunzo kuhusu maswala ya Uhasibu, Ukaguzi wa ndani na akili Mnemba (AI) yatafanyika kwa muda wa siku tatu katika ukumbi wa **St Gaspar jijini Dodoma tarehe 21 hadi 23 Januari, 2026** kuanzia saa mbili kamili asubuhi. Mafunzo hayo ni mahususi kwa **Watendaji ambao ni Mameneja, Wahasibu, Wakaguzi wa ndani, Wajumbe wa Bodi** na mtu yoyote ambaye atapenda kupata ujuzi kwenye hayo.

4. Kila mshiriki anatakiwa kuchangia ada ya Tshs 350,000 ambayo inajumuisha gharama ya mafunzo ya siku tatu, ukumbi, chai na chakula cha mchana wakati wa mafunzo. **Malipo hayo yatalipwa kupitia nambari ya malipo ya Serikali** itakayotolewa baada ya kuthibitisha ushiriki wako kwa kuwasiliana na RCA au mratibu wa mfunzo (CPA Gabriel Msuya) kupitia **nambari ya simu 0762 389 616** au barua pepe ***gabriel.msuya@coasco.go.tz***

5. Tafadhali unaombwa kuhakikisha uthibitisho wa ushiriki wako kwa wakati na malipo yafanyike mnamo au kabla ya **tarehe 15.01.2026.**

Natanguliza shukrani,

Pamoja tujenge Uchumi.

**CPA Gabriel L. Msuya**
**KNY: MKURUGENZI MKUU**

*COASCO, 2 Barabara ya Hatibu, 41103 Madukani, S. L. P. 761, Dodoma, Simu: +255 026 2321485/+255 026 2321704, Nukishi +255 026 2321 486, Barua pepe: info@coasco.go.tz, Tovuti: www.coasco.go.tz*